

Learning by Ear 2009
Migration - Lampedusa
Author: Sandra Petersmann

Learning by Ear 2009

Migration – Lampedusa

Author: Sandra Petersmann

Editors: Katrin Ogunsade/Jan-Philipp Scholz

Translator: Tony Dunham/Jan-Philipp Scholz

Presenters:

1 announcer, male or female (intro, outro, connection)

1 narrator, female (text)

Sound Bites:

(total: 4 female voices, 2 male voices)

- Barbara Molinario, female (middle-aged)
- Carlotta Santarossa, female (middle-aged)
- Bernadino de Rubeis, male (middle-aged)
- Giusi Nicolini, female (middle-aged)
- Dagwami Yimer, male (around 30)
- Paola la Rosa, female (middle-aged)

Intro:

Hujambo na karibu kwenye makala nyingine ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu uhamiaji. Kwenye kipindi hiki tunakupeleka moja kwa moja hadi Lampedusa, kisiwa kilichopo kusini mwa Italia. Kisiwa hiki kidogo kipo katika bahari ya Mediterranean kati ya Tunisia na Sicily. Kila mwaka takriban wakimbizi elfu kumi kutoka Afrika hupitia kwenye kisiwa hiki na kuingia Ulaya. Lakini wakimbizi hawa hawatajikani. Serikali ya Italia inazidi kuweka sheria kali ili kumaliza tatizo hili la uhamiaji haramu. Wakaazi wa Lampedusa wanakumbana na maamuzi ya sheria hiyo mpya katika maisha yao ya kila siku, kama ripota wetu Sandra Petersmann anavyoripoti.

1. SFX waves, seagulls

Mawimbi ya bahari ya Mediterranean yanapasua katika kisiwa kidogo kilichopo baina ya miamba miwili. Maji yametulia, yana metameta kwenye miale ya jua.

2. SFX waves, seagulls

Kuna watu 70 ndani ya Jahazi ijapokuwa hamu yao si kuangalia uzuri wa Lampedusa. Wahamiaji hao walio choka wamehatarisha maisha yao kwenye safari hiyo ya kuisimua kupitia Libya ndani ya mashua ndogo. Barbara Molinario kutoka shirika la umoja wa mataifa linaloshughulikia wakimbizi (UNHCR) anakisia kuwa kila mmoja wa wasafiri hao amelipa

Learning by Ear 2009

Migration - Lampedusa

Author: Sandra Petersmann

kiasi cha dola 1500 kwa watu wanaofanya biashara ya kusafirisha watu kimagendo.

3. Sound bite Molinario (engl.):

„Mara nyingine mkimbizi kutoka Somalia au Eritrea analazimika kufanya kazi kwa miaka miwili, kulipia deni la safari hiyo ambayo ni ghali mno, wanalazimika kufanya kazi kwenye nchi mbali mbali. Kusafiri baharini ndio sehemu ya mwisho ya safari yao hiyo baada ya kupitia mambo mengi magumu. Wanasema hupata dhiki kubwa wakati wa kuvuka jangwa la Sahara wakiwa wamejazwa ndani ya magari madogo bila hata maji ya kunywa ya kutosha. Huu ndio wakati ambapo wengi wao huwa wanafariki.

4. SFX waves, seagull

Maafisa nchini Italia huwagawa wageni katika makundi mawili. Waafrika wanaotoka katika nchi zilizo kusini ya jangwa la Sahara ambao wanawekwa kwenye kundi la wakimbizi wenye kutafuta hifadhi na hao hupelekwa kwenye kisiwa cha Sicily au ndani ya Italia kwenyewe. Waafrika kutoka eneo la Kaskazini nao wanawekwa kwenye kundi la wahamiaji haramu na hivyo basi wao hubaki kwenye kisiwa hicho kama Carlotta Santarossa wa Shirika la Kimataifa la Uhamiaji anavyoeleza:

5. Sound bite Santarossa (engl.):

„Kwa sasa kituo hicho kimejaa watu kupita kiasi. Hali ya maisha hapo si nzuri hata kidogo. Ni vigumu kuweza kuwahifadhi watu wengi kwa muda mrefu. Vituo vingine vya utambulisho nchini Italia havina idadi kubwa ya wakimbizi kama hiki.

6. SFX waves, seagull

Kituo cha mapokezi kwa sasa kinatumika pia kama kituo cha kuwarudisha watu makwao, kwa sababu jengo la kuendesha shughuli za kuwarudisha watu makwao bado halijamalizika kujengwa. Awali wakimbizi walikaa kwenye kisiwa hiki kwa siku chache tu lakini siku hizi wanaweza kuzuiliwa hadi miezi sita.

7. Sound bite de Rubeis (ital.):

„Tumeieleza Italia, Ulaya na hata Ulimwengu mzima kwa jumla, kwamba hatutaki kuwa na kisiwa kilicho sawa na jela kilicho na kambi kubwa ya kuwarudisha wakimbizi makwao. Sote hapa tunategemea utalii, tunatarajia kuwa kutafanyika mazungumzo.“

Meya wa Lampedusa Bernardino de Rubeis amekwama . Anafurahia masharti makali ya uhamiaji na mpango wa kuwarudisha wahamiaji makwao unaoendeshwa na serikali ya Italia – iwapo tu mambo hayo hayafanyiki katika kisiwa chake.

8. SFX conversation Isole Pelagie

Wenye mahoteli na mikahawa wanaitishia serikali ya mjini Roma hata kwa vita kwa sababu wanasema watalii hawaonekani, isipokuwa wageni wanao onekana kwa wingi katika kisiwa hicho ni zaidi ya polisi 1000 na wanajeshi ambao wamepelekwa huko kwa wingi.

9. SFX conversation women after mess/ fade under

Baada ya misa ya asubuhi, wanawake wazee wamesimama nje ya kanisa. Wanazungumza kuhusu wakimbizi waliokuja kwa mashua na ambao sasa wanahitaji msaada. Wanazungumzia pia kuhusu vitendo vya ubakaji, ukahaba na biashara ya madawa ya kulevya.

10. SFX church bells and conversations/ fade under

Kisiwa kidogo cha Lampedusa kina wakaazi wasiozidi 6,000. Hofu ya ongezeko la wageni na vitendo vya uhalifu inaongezeka. Ijapokuwa wakimbizi hawaonekani katika maisha ya kila siku katika kisiwa hicho kwa sababu wamezuiliwa.

11. SFX church bells and conversations/ fade under

Giusi Nicolini anasimamia hifadhi ya viumbe katika kisiwa cha Lampedusa , yeye ni mwanaharakati wa kundi dogo linalo tetea haki za binadamu, kundi hilo linaandaa malalamiko kukipinga kituo cha kuwarudisha watu makwao. Malalamiko hayo yatawasilishwa kwa miji ya Rome na Brussels.

12. Sound bite Nicolini (ital.):

„ Katika maswala ya kulinda mazingira Umoja wa Ulaya wakati wote unatilia mkazo kutiliwa maanani watu wanaoathirika. Ninapotaka kutekeleza miradi yangu ya hifadhi ninatilia maanani madhara yanayoweza kuwaathiri watu. Lakini kuhusu uhamiaji hakuna anaejali. Serikali ya Italia ina uhuru wa

kutosha juu ya swala hilo. Umoja wa Ulaya haujali haki za binadamu za wakimbizi wala haki za wakaazi wa kisiwa hicho.“

Music

Connection /Narrator:

Dagwami Yimer ni kijana wa Kiafrika miongoni mwa vijana waliohatarisha maisha yao kwa sababu ya kuja Ulaya. Mwanafunzi huyo wa sheria alikuwa na miaka 27 wakati alipoondoka nchini mwake, ulikuwa ni wakati wa msimu wa baridi mnamo mwaka 2005. Alipitia Sudan hadi Libya. Alinaswa na mtego wa watu wenye kufanya biashara ya kuwatorosha watu, alikamatwa na askari wa Libya na kisha kurudishwa. Alitelekezwa jangwani bila hata maji ya kunywa. Licha ya yote hayo alirudi tena katika pwani ya Libya na kuhatarisha maisha yake katika safari hiyo ya hatari kwenye mashua ndogo kupitia bahari ya Mediterranean. Msimu wa kiangazi mwaka 2006 – baada ya kuteseka kwa miezi mingi – alifika katika kisiwa cha Lampedusa. Hivi karibuni, Dagwami Yimer alirudi tena kisiwani kwa mara ya kwanza. Kuja kuonyesha watu filamu kuhusu safari za kila siku zinayofanywa na makundi ya vijana wanaodai kwamba wanakimbia hali ngumu ya maisha kutoka Afrika.

13. O-Ton Atmo (Film)

Unaweza kuisikia pini ikidondoka, jinsi ukumbi wa kanisa ulivyonyamaa. Macho ya watu yameganda kwenye ubao wa sinema. Takriban wakaazi

Learning by Ear 2009
Migration - Lampedusa
Author: Sandra Petersmann

50 wa kisiwa hicho wamefika kuiona filamu hiyo, “ kama binadamu duniani” kwenye filamu hii vijana wahamiaji kama vile Dagmawi Yimer wanaeleza kuhusu safari zao. Safari hii huchukua kama miezi 6 hadi mwaka mmoja kukamilika.

14. O-Ton Atmo (Film)

Vijana wanaume kwa wanawake wanaelezea jinsi walivyopigwa, kuibiwa, kukamatwa, kubakwa na hata kutelekezwa jangwani. Wanaeleza kwa uchungu huku machozi yanawatoka . Wanaelezea waliyotendewa kutokana na maamuzi holela ya maafisa na watu wanaofanya biashara ya kuwatorosha watu.

15. O-Ton Atmo (Film)

Dagmawi Yimer kutoka Ethiopia ametengeneza filamu hiyo pamoja na watengeneza sinema wawili wa Kitaliani ambao wamekuwa marafiki. Sasa anaishi mjini Rome, lakini hajasahau kamwe muda mfupi aliokuwa katika kisiwa cha Lampedusa katika msimu wa kiangazi mwaka 2006 baada ya kufaulu katika safari yake ngumu.

16. O-Ton Dagmawi (engl.):

„Nilikuja hapa kwa mashua tena bila viatu. Sasa nimerudi hapa nikiwa nimevaa viatu tena nimekuja kwa ndege. Sijui nieleze vipi hisia zangu. Nimeonyesha filamu hii katika maeneo mengi hapa nchini Italia lakini wakati huu ambapo nimerudi hapa Lampedusa, ni mara ya kwanza nimepandwa na hisia kali.“

Dagmawi, ambae kila mtu anamuita Dug, alikuwa na miaka 27 wakati alipoamua kuondoka Ethiopia.

17. O-Ton Dagmawi (engl.):

„Niliondoka kwa sababu nilivunjika moyo kuendelea kuishi katika nchi ambayo haina demokrasia. Nilivunjika moyo na sikuweza kuendelea na masomo yangu ya chuo kikuu. Na hiyo ndio sababu yangu kubwa ya kuipinga serikali. Niliona ni heri nifanye safari kama ile.“

Filamu hiyo pia ni sehemu ya upinzani na hasa dhidi ya Libya na wazo la nchi za umoja wa ulaya la kutaka kuifanya Libya kuwa ndio kituo cha kuwapeleka wahamiaji wote wanaokimbia kutoka kwenye nchi zao.

18. O-Ton Dagmawi (engl.):

„Jambo baya zaidi ni Kontena. Serikali inakurudisha ukiwa ndani ya Kontena kupitia kwenye jangwa, kwenye jangwa la Sahara la Libya bila hata kujali utu wako – yaani kama mnyama.“

Dag ameepuka salama baada kupitia mateso yote hayo Kontena, jangwa, na safari kupitia bahari ya Mediterranean. Haijulikani ni watu wangapi wameilipia safari hiyo kwa maisha yao. Watalaamu wanakisia kuwa kati ya wakimbizi wanne mmoja tu ndio hunusurika kifo kwenye safari ya aina hiyo ..

19. O-Ton Dagmawi (engl.):

„Kwa wale wanaopanga kufanya safari ya aina hiyo. Siwezi kuwakataza. Au siwezi kusema msijaribu. Angalau mimi nilinusurika na ninaeleza

yaliyonifika. Kwa sababu wengi watasema kama mimi niliweza basi na wao watafaulu.“

Italia, Ulaya. Ndoto ya Ardhi yenye ahadi. Lakini ukweli ni tofauti kabisa.

20. O-Ton Dagmawi (engl.):

„Lazima ufanye bidii ndio ufikiriwe. Lazima uanzie chini kabisa ndio utambuliwe kuwa na wewe pia ni binadamu. Bila kufikia kiwango fulani wewe utabakia kuwa namba, mhamiaji au nigger tu. Hayo ndio niliyakuta nilipofika huku Italia, Ulaya hukaribishwi.“

Dagmawi kutoka Ethiopia sasa ana miaka 31. Mjini Rome anawasaidia wahamiaji na anatengeneza filamu kuhusu mikasa inayowapata. Amepata mpenzi anaitwa Elena.

21. O-Ton Dagmawi (engl.):

„Maisha siyo rahisi. Hata kwa raia wa Ulaya wenyewe mambo siyo rahisi kabisa. Mimi ninafuraha kuwa na msichana ninaempenda. Mtu akiniuliza kama mpenzi wangu ni Mtaliani? Mimi huwa sijibu swali hilo. Kwa sababu nimekutana na msichana ambaye sio Mtaliani.“

22. O-Ton Atmo (Applaus nach Film)

Kama mwanadamu duniani – filamu hiyo imewavutia sana watazamaji katika kisiwa cha Lampedusa. Onyesho hilo ndani ya kanisa liliandaliwa na wakili Paola La Rosa. Paola ni mzaliwa wa Palermo na ameishi katika kisiwa hicho kidogo kilicho katika bahari ya Mediterranean kwa miaka 10. Takriban wahamiaji elfu 32 waliishi katika kisiwa hiki mwaka jana.

23. O-Ton Paola (engl.):

„Kwa miaka kumi nimeona sura hizi. Sura za watu weusi wakipita karibu nami, ndani ya basi au wakiwasili kwa mashua. Lakini sikuwa nimepata fursa ya kuzungumza hata na mmoja wao.“

24. O-Ton Atmo (Gespräche nach Film)

Lampedusa ina takriban wakaazi 6,000. Ni wakaazi wachache tu ndio hupata fursa ya kuwasiliana na wahamiaji ambao wanaishi kwenye kambi za wakimbizi kabla ya kuachiwa kwenda kuishi kisiwani. Wakati Paola alipopata habari kuhusu mradi wa filamu, mara moja alishika simu..

25. O-Ton Paola (engl.):

„Nina hamu ya kukutana na Dag ninataka kumgusa pia, na kuiona sura yake na macho yake, ninataka kuzungumza na yeye na pia kuisikia sauti yake kwa sababu yeye ni mtu sio namba.“

Outro:

Na hiyo ndio ilikuwa hadithi ya Dagwami Yimer kutoka Ethiopia ambae alikwama wakati akiwa mkimbizi katika kisiwa cha kusini mwa Italia cha Lampedusa. Ameyakusanya mawazo yake na kutengeneza filamu. Na mpaka hapo ndio tumeakmilisha kipindi chetu kwa leo katika makala ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu uhamiaji. Ukitaka kujifunza zaidi tembelea kwenye mtandao wetu. Anuani yetu ni: www.dw-world.de/lbe
Sina shaka utajiunga nasi tena wakati mwingine. Kwaheri.